

## MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



### TAARIFA KWA UMMA

11 Septemba, 2018

#### TAARIFA YA UWEPO WA DAWA BANDIA YA VIDONGE YENYE JINA DUO-COTECXIN KATIKA SOKO

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa inapenda kuutaarifu umma kuwa imebaini uwepo wa toleo (batch) la dawa bandia ya binadamu ya vidonge aina ya Duo-cotexcin kwenye soko inayodaiwa kutengenezwa na kiwanda cha Zhejiang Holley Nanhu Pharmaceutical Co., Limited, China.
2. Kasha la dawa hiyo linaonesha namba ya toleo kuwa ni 170259, tarehe ya kutengenezwa ni 25 Februari, 2017 na tarehe ya kuisha muda wa matumizi ni Februari, 2019.
3. Utufauti wa dawa bandia iliyokamatwa na dawa halisi iliyosajiliwa na TFDA umeainishwa katika **jedwali** hapa chini:-

Na.	Dawa halisi	Dawa bandia
3.1	Tarehe ya kutengenezwa, tarehe ya mwisho wa matumizi na namba ya toleo <b>zipo</b> katika kasha la ndani ( <i>blister/primary pack</i> ).	Tarehe ya kutengenezwa <b>haipo</b> katika kasha la ndani ( <i>blister/primary pack</i> ).
3.2	Maandishi ya namba ya usajili yaliyochapishwa kwenye kasha la nje ( <i>secondary pack</i> ) yamepangika vizuri katikati ya kasha.	Maandishi ya namba ya usajili yaliyochapishwa kwenye kasha la nje ( <i>secondary pack</i> ) <b>hayajapangika</b> vizuri.
3.3	Karatasi ambatishi ya dawa ( <i>package insert</i> ) <b>ina</b> nembo ya Holley-Cotec katika pande zote mbili za maelezo ya lugha ya kiingereza na kifaransa.	Nembo ya Holley-Cotec katika <i>package insert</i> <b>haipo</b> katika upande wa lugha ya kiingereza
3.4	Rangi ya vidonge ni bluu <b>iliyokolea</b> zaidi.	Rangi ya vidonge ni bluu <b>isiyokolea</b> ( <i>light blue</i> ).
3.5	Kasha la ndani ( <i>primary pack/blister</i> ) <b>linang'aa</b> .	Kasha la ndani ( <i>primary pack/blister</i> ) <b>limefifia</b> .
3.6	Namba ya toleo iliyopo kwenye kasha la ndani inafanana na iliyopo kwenye kasha la nje.	Namba ya toleo iliyopo kwenye kasha la ndani (toleo namba 150644) ni tofauti na iliyopo kwenye kasha la nje (toleo Na.170259).

4. Jumla ya makasha 22 ya vidonge 9 kila moja ya dawa bandia yalikutwa kwenye maduka mawili ya dawa ya Bi.Julieth Francis Madrina na Bw. Swaib Abrahaman eneo la Kinondoni Mkwajuni. Watuhumiwa wamefikishwa kituo cha polisi ili taratibu zingine za kisheria ziweze kuendelea.

5. Kutokana na kubainika kwa toleo la dawa hiyo bandia, Mamlaka inautahadharisha umma, wafanyabiashara pamoja na watoa huduma za afya mambo yafuatayo:-
  - a) Kuangalia kwa makini makasha ya dawa ya Duo-cotecxin wakati wanapopewa kwenye maduka ya dawa na vituo vya kutolea huduma za afya ili kubaini toleo la dawa bandia iliyokamatwa.
  - b) Kurudisha dawa walipozinunua ili taratibu zilizowekwa ziweze kuendelea.
  - c) Watoa huduma za afya wote ikiwa ni pamoja na maduka ya dawa yaliyouza dawa husika watoe taarifa TFDA ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.
6. Wananchi mnaombwa kuendelea kutoa taarifa pale mnapobaini uwepo wa dawa duni na bandia kwenye soko ili kulinda afya zetu.

**Imetolewa na;**

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Chakula na Dawa,  
S.L.P 77150,  
Dar es Salaam.**

**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751/**

**658 445222/777 700 002/685 701735**

**Nukushi: +255 22 2450793**

**Barua pepe: [info@tfda.go.tz](mailto:info@tfda.go.tz)**

**Tovuti: [www.tfda.go.tz](http://www.tfda.go.tz)**